**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**Juni, 2023**

**Dodoma**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**Namba za Simu**

**Mkuu wa Shule 0655 578 940**

**Makamu Mkuu wa Shule. 0625 986 182**

**Matron/Patron 0620 39 41 67**

**Shule ya Sekondari MAFISA**

**S.L.P. 24 SONGE – KILINDI, TANGA**

**Tarehe 13/6/2023**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ________________________________________**
**S.L.P ____________________**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MAFISA HALMASHAURI YA KILINDI MKOA TANGA MWAKA 2023/2024**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2023. na atasoma tahasusi ya HKL

Shule hii ipo Mkoa wa Tanga katika wilaya ya Kilindi,Shule ipo kijiji cha Mafisa kilometa 21 kutoka makao makuu ya Wilaya ya KILINDI –SONGE. Kwa Wanafunzi wanaotokea DAR ES -SALAAM watapanda mabasi yanayoelekea SONGE na watafikishwa kwenye kijiji cha MAFISA mahali ilipo shule hii,kwa wale wanaotokea mikoa ya ARUSHA NA KILIMANJARO watashuka kwenye mji wa HANDENI na kupanda mabasi yanayoelekea SONGE na kushushwa katika kijiji ya MAFISA ilipo shule hii.Kwa wale wanaotokea Mikoa ya Nyanda za juu kusini,Kanda ya Ziwa na Kanda ya Kati watafika DODOMA na kupanda mabasi yanayopitia njia ya Gailo au Kiteto watafikishwa kwenye kijiji cha MAFISA ilipo shule hii.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe 14/8/2023, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 13/08/2023. Mwisho wa kuripoti ni tarehe 31/08/2023

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### 2.1 Sare za Shule

i. Sare ya shule hii ni SURUALI 2 RANGI YA KIJIVU. Yenye MARINDA MAIWILI kila upande na isiwe ya kubana (upana iwe inch 15)
ii. Mashati 2 meupe yenye mikono mirefu na isiwe ya kubana
iii. Sare ya Michezo ni Track suit dark blue na raba rangi yeyote;
iv. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;
v. Soksi jozi mbili nyeusi
vi. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali;
vii. Sweta 1 rangi ya kijivu yanapatikana karibu na mazingira ya shule kwa bei ya tsh. 14,000/= anaruhusiwa kuja na koti jeusi zito la ziada lisilo kua na kofia kwa sababu ya Baridi.
viii. Nguo za kushindia tisheti 2 za light blue na suruali 2 nyeusi zisiwe za kubana
ix. Tai 2 za kijivu
x. Tisheti 1 ya shule inapatikana mazingira karibu na shule kwa bei ya Tsh. 15,000/=

### 2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

i. Mwanafunzi aje na nakala (copy) 1 ya vyeti (kuzaliwa, CSEE result slip)
ii. Madaftari 7 ya counterbook Quire 3 AU Quire 4;
iii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;
iv. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika ya HKL
   - Kamusi ya KISWAHILI
   - Advanved Learners Dictionary
   - Vitabu rejea kwa masomo ya HISTORY 1&2, KISWAHILI 1 NA ENGLISH LANGUAGE 1
   - Tahakiki kwa masomo ya KISWAHILI 2 na English langauge 2
v. Godoro kwa wanafunzi wa Bweni liwe na vipimo vya Futi mbili na nusu kwa Sita (2.5 *6 ft) na unene wa inch 4. Mzazi aje na godoro hilo au linapatikana karibu na mazingira ya shule kwa bei ya Tsh. 38,000/=

vi. Mashuka Jozi 2 rangi ya light blue, blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1.
vii. Nguo za ndani za kutosha;
viii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
ix. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
x. Kwanja 1, jembe 1, mifagio 2 wa ndani na nje
xi. Aje na sanduku la bati kwaajili ya kutunzia vifaa vyake

**ANGALIZO**: Mwanafunzi apangiwe kuleta kifaa kulingana na mazingira ya shule na tahasusi anayosoma.

**2.3 Michango mbalimbali**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

FEDHA HIZI ZA MICHANGO ZILIPIWE KUPITIA AKAUNTI YA SHULE AMBAYO NI

**NMB 4261100026**
JINA LA AKAUNTI **MAFISA SECONDARY SCHOOL CAPITATION**

**NB: Mwanafunzi aje na BIMA YA AFYA inayofanya kazi au aje na fedha taslimu Tsh. 20,000/= kwa kila mwaka wa masomo kwa ajili ya kutengenezewa BIMA YA AFYA.**

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule .......................................**

**Jina la Mkuu wa Shule . HASSANI O. HASSANI**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule.....................................**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0655 578 940/ 0613 081 508**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0625 986 182**
- **Mwandamizi Taaluma 0692 69 22 22**
- **Mwandamizi Malezi 0620 39 41 67**